



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia watanzania wenye sifa kuomba kazi za muda kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Waombaji wanatakiwa kuwa ni Watanzania wenye sifa zifuatazo;

(a) Sifa za Msingi:-

1. Umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45.
2. Elimu ya kidato cha nne na kuendelea pamoja na ujuzi wa kutumia kompyuta.
3. Awe na uwezo wa kutambua matatizo ya kompyuta ya *hardware* na *software* na kuyatatua.
4. Awe na uwezo wa ku-install program za kompyuta na kutoa msaada wa kiufundi wa TEHAMA kwa watumiaji.
5. Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai
6. Awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yenye usimamizi mdogo

(b) Sifa za ziada:-

- Waombaji wenye uzoefu wa kutumia BVR Kits waliowahi kufanya kazi vizuri wakati wa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015 watapewa kipaumbele.
- Wenye shahada ya TEHAMA watapewa kipaumbele.

Barua ya maombi ya kazi ionyeshe anuani kamili, namba ya simu na iambatishwe na nakala ya vyeti vyote vya elimu na mafunzo, pamoja na wasifu wa mwombaji (CV) ikionyesha wadhamini wawili.

Maombi yatumwe kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, S.L.P 10923 DAR ES SALAAM kupitia necrecruitment@nec.go.tz kabla ya tarehe 02/06/2019.


Mabamba Rajab Moses

Kny: MKURUGENZI WA UCHAGUZI